# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la 3



Taasisi ya Elimu Tanzania

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi
## Darasa la Tatu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 562

Jina la Chapisho: Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-317-5

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tatu katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2015.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 1 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018
Toleo la Pili 2021

ISBN 978–9987–09–317–5

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 170 / +255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 2 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi** ........ iv

**Shukurani** ........ v

**Sura ya Kwanza**
Mazingira yetu ........ 1

**Sura ya Pili**
Hali ya hewa ya mazingira yetu ........ 16

**Sura ya Tatu**
Utamaduni wetu ........ 22

**Sura ya Nne**
Uhusiano mwema ........ 31

**Sura ya Tano**
Viongozi wa nchi yetu ........ 43

**Sura ya Sita**
Kusoma ramani ........ 52

**Sura ya Saba**
Mfumo wa jua ........ 59

**Sura ya Nane**
Kutunza rasilimali zetu ........ 62

**Sura ya Tisa**
Uzalishaji mali ........ 70

**Sura ya Kumi**
Kutambua fursa katika maeneo mbalimbali ........ 76

**Jaribio** ........ 81

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki cha Maarifa ya Jamii ni kitabu cha kwanza cha mwanafunzi. Huu ni mfululizo wa vitabu vitano vya somo hili. Vitabu hivyo ni vya darasa la tatu, nne, tano, sita na saba. Kitabu kimeandaliwa ili kusaidia kujenga umahiri katika somo la Maarifa ya Jamii. Aidha mada zilizoelezwa zinahusu mazingira, uzalendo, matumizi ya ramani na elimu ya anga. Pia, kanuni za uchumi katika uzalishaji mali zimeelezwa.

Uandishi wa kitabu umezingatia mahitaji ya mwanafunzi katika kujenga umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Hivyo, kimesheheni matini za kusoma. Matini hizo zimeandikwa katika mtindo wa ushairi, majigambo, hadithi, majibizano na vifungu vya maneno na kufafanuliwa kwa picha na michoro.

Maswali yaliyomo kwenye kitabu hiki yatamwezesha mwanafunzi kufikiri na kujenga umahiri uliokusudiwa. Aidha, kazi anazopewa mwanafunzi zitamwezesha kupata uelewa wa kina na kutumia umahiri uliojengwa katika maisha yake ya kila siku.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 4 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
***Taasisi ya Elimu Tanzania***

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 6 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Mazingira yetu

Ulipokuwa darasa la pili ulijifunza kutambua wanyama wa aina mbalimbali. Aidha, ulijifunza kutambua viumbe hatarishi katika mazingira. Katika sura hii utajifunza vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule na nyumbani. Vilevile, utajifunza kufanya usafi wa darasa na usafi wa mazingira ya shule.

### Vitu vinavyopatikana katika mazingira


Mazingira ni vitu mbalimbali vinavyomzunguka mwanadamu. Vitu hivyo vinaweza kuwa katika mazingira ya nyumbani au mazingira ya shuleni. Vitu hivi vinaweza kugawanyika katika makundi mawili. Makundi hayo ni vitu vilivyo hai na vitu visivyo hai.


### A. Vitu vilivyo hai

Vitu vilivyo hai ni kama watu, ndege, ng'ombe na miti.









FOR ONLINE USE ONLY





Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 1 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## B. Vitu visivyo na uhai

Vitu visivyo na uhai ni kama vile nyumba, reli, barabara na mawe.








## Vitu vinavyopatikana katika mazingira ya nyumbani

Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 1** Vitu vinavyopatikana katika mazingira ya nyumbani

### Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vitu vitatu vinavyopatikana katika mazingira ya nyumbani. (a) ________ (b) _______ (c) _________.
2. Taja vitu vitatu ambavyo vipo nyumbani kwenu lakini havipo katika picha. (a) _________ (b) _______ (c) _________.
3. Taja vitu vinne vyenye uhai ambavyo hupatikana nyumbani. (a)_________ (b)_________ (c)_________ (d)_________.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule

Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 2** Mazingira ya shule

### Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vitu vitatu visivyo na uhai vinavyoonekana katika picha.
2. Vitu gani viko shuleni kwako ambavyo vinafanana na vile vilivyoko katika picha?
3. Taja faida mbili za miti katika mazingira ya shule.
   (a) ____________ (b)_____________.



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 3 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Taja vitu vitatu vilivyoko katika mazingira ya shule yako.
   (a) ____________
   (b) ____________
   (c) ____________.
5. Chora vitu viwili vinavyopatikana katika mazingira ya shule.

## Zoezi la 3

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Mazingira ni ______________________
   (a) magari yaliyo shuleni.
   (b) vitu vinavyomzunguka mwanadamu. (     )
   (c) wanyama.
2. Vitu vinavyopatikana katika mazingira vimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni______________
   (a) barabara na nyumba.
   (b) vitu vilivyo hai na visivyo hai. (     )
   (c) vinavyoruka na visivyoruka.
3. Vifuatavyo ni vitu vilivyo na uhai _______________
   (a) mawe na ndege.
   (b) mwanadamu na wanyama. (     )
   (c) miti na magari.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 4 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mazingira ya Shule ya Msingi Kisomola

Rabia na Kaluza wanasoma darasa la tatu katika Shule ya Msingi Kilimani. Siku ya Jumatatu walipeleka barua katika shule ya Kisomola. Walipokaribia waliona mazingira mazuri kuzunguka shule.

Soma mazungumzo kati ya Rabia na Kaluza, kisha jibu maswali.

| | |
|---|---|
| **Kaluza** | Naona tumekaribia shule ya Kisomola. |
| **Rabia** | Kweli tumefika, hata miti na ndege wanatulaki kwa furaha. |
| **Kaluza** | Aaah! kumbe wana miti mingi ya kivuli kuliko sisi. Miti yao inaleta hewa nzuri. |
| **Rabia** | Jamani, angalia bustani zao za maua zimepangwa kwa ustadi. Zinapendezesha shule. |
| **Kaluza** | Eeeh! Angalia kibao cha shule kimeandikwa jina la shule kwa ustadi mkubwa. |
| **Rabia** | Pia, wana uwanja mkubwa wa michezo, uleee! Unauona? |
| **Kaluza** | Rabia umeona ile bustani ya mboga inavyopendeza? |
| **Rabia** | Ni kweli nimeona,watakuwa wanauza mboga na kupata fedha nyingi. |
| **Kaluza** | Je, umeona majengo ya madarasa yao na ofisi za walimu zilivyo nzuri? |
| **Rabia** | Nimeona, tena zimepakwa rangi na kuchorwa ramani na vitu mbalimbali vya kuvutia. |
| **Kaluza** | Tena wenzetu wana kisima cha maji. |
| **Rabia** | Ni kweli, ndio maana bustani zao za maua na mboga zimestawi vizuri. |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 5 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Rabia na Kaluza walifurahia mazingira mazuri ya shule ya Kisomola. Baada ya kufikisha barua, waliahidi kurudi tena shuleni hapo kujifunza juu ya mazingira.

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vitu viwili vilivyopo katika shule ya Kisomola lakini havipo shuleni kwako.
   (a) ____________
   (b) ____________.
2. Taja vitu vitatu vilivyokuvutia katika mazingira ya shule ya Kisomola.
   (a) ______________
   (b) ______________
   (c) ______________.
3. Taja mambo matatu yanayopaswa kufanywa ili kuboresha mazingira ya shuleni kwako.
   (a) ______________
   (b) ______________
   (c) ______________.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako kuchunguza mazingira ya shule yenu. Orodhesha vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule yenu.



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 6 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutunza mazingira ya shule

Tumeona vitu vilivyoko katika mazingira ya shule. Ni muhimu kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi. Tunatunza mazingira ya shule kwa kufanya usafi na kurekebisha maeneo yaliyoharibiwa. Aidha, tunapanda na kutunza miti, nyasi na maua. Pia, tunadhibiti takataka na kufanya usafi wa madarasa, vyoo na majengo.

## Usafi wa darasa

Ni muhimu kuweka darasa katika hali ya usafi wakati wote. Usafi wa darasa hufanywa na wanafunzi kwa zamu. Usafi huu hufanyika kwa kushirikiana.

Tazama picha, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 3** Wanafunzi wakifanya usafi wa darasa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 5

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vitendo viwili vinavyofanyika katika picha.
   (a) _______ (b) _______.
2. Taja vitendo vitatu vya usafi vinavyofanyika darasani kwako. (a) _______ (b) _______ (c) _______.
3. Nini kitatokea ikiwa darasa halitafanyiwa usafi?
4. Taja faida nne za kufanya usafi wa darasa lako.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _____.
5. Unashiriki kazi gani wakati wa kufanya usafi darasani siku ya zamu yako?

## Mashindano ya usafi wa madarasa

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.

Ijumaa ni siku ya mashindano ya usafi wa madarasa katika shule yetu. Usafi huo hufanyika baada ya masomo. Ijumaa iliyopita tulishirikiana kufanya usafi wa darasa letu. Wakati tukifanya usafi Juma alisema, "Ni muhimu kufanya usafi darasani ili kupendeze". Helena alichukua kitambaa akaanza kufuta vumbi akisema, "Tufute vumbi ili tusichafue nguo". Halima naye alichukua ufagio mrefu na kuondoa tandabui. John alisema, "Halima, umefanya vizuri kuondoa tandabui maana wanaharibu mazingira ya darasa. Takataka pia huwa maficho ya mbu na wadudu wengine". Doto aliongeza kuwa, "Tusipoondoa maficho ya mbu watatuuma na kutuambukiza malaria". Mariamu na Faraja walisafisha meza, kiti cha mwalimu na kabati la vitabu. Kisha, tulishirikiana sote kufagia na kupiga deki darasa letu. Tulitumia dekio, ndoo, maji na sabuni kudeki darasa.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 8 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Darasa letu lilipokauka tulipanga madawati yetu vizuri. Tulihakikisha kuwa tunaacha nafasi ya kutosha kati ya dawati na dawati.

Walimu na viranja walipopita kukagua usafi, darasa letu lilishinda tukawa wa kwanza. Tulipata zawadi ya ngao. Tulishangilia kwa furaha. Kwa pamoja tulikubaliana kuwa usafi wa darasa letu uwe ni suala la kila siku.

## Zoezi la 6

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vifaa vinne vilivyotumika kufanyia usafi wa darasa.
   (a) ________ (b) ________ (c) ________ (d) ________.
2. Taja faida mbili za kufanya usafi darasani.
   (a) ________ (b) ________.
3. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu walishinda zawadi ya usafi?
4. Kwa nini tunapanga madawati kwa mistari na kuacha nafasi ya kutosha?

## Kazi ya kufanya

**Jibu maswali haya.**

1. Taja sifa ya darasa safi.
2. Eleza mambo manne ya kufanya wakati wa kufanya usafi wa darasa.
3. Chora vifaa vinne mnavyotumia kufanyia usafi wa darasa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama picha, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 4** Wanafunzi wakifanya usafi wa mazingira

## Zoezi la 7

**Jibu maswali haya.**

1. Ni shughuli gani za utunzaji wa mazingira zinazoonekana katika picha?
2. Taja vifaa vitatu vya usafi wa mazingira vinavyoonekana katika picha.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______.
3. Taja shughuli mbili za kutunza mazingira zinazofanyika shuleni kwako.
   (a) ______ (b) ______.
4. Kwa nini tunahitaji kutunza mazingira ya shule?



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 10 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Usafi wa mazingira katika Shule ya Msingi Juhudi

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.

Amani ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Juhudi. Wanafunzi wa shule ya Juhudi wana nidhamu sana. Amani na wenzake wanawahi shuleni mapema asubuhi. Wanafika shuleni saa kumi na mbili na nusu asubuhi. Wanapofika shuleni hupangiana maeneo ya kufanya usafi wa shule kwa kushirikiana. Kazi za usafi wanazofanya ni kuokota takataka na kuzitupa katika shimo. Vilevile, hufagia barabara na njia za kupita katika eneo la shule. Aidha, hufyeka nyasi ndefu kwa kutumia mafyekeo. Baadaye hupalilia maua kwa kutumia jembe na kumwagilia maji. Kisha, wanamwagilia maji kwenye miti midogo. Baada ya usafi, wanajipanga kwenye mistari mbele ya shule kusikiliza matangazo. Kisha, wanaingia darasani kuanza masomo.

### Zoezi la 8

**Jibu maswali haya.**

1. Taja shughuli nne zinazofanyika katika habari uliyosoma.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______.
2. Ni vifaa gani vitatu vilitumika kufanyia usafi katika habari uliyosoma? (a) _______ (b) _______ (c) _______.
3. Amani na wenzake hufanya nini mara baada ya kufika shuleni?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kupanda miti, nyasi na maua

Miti, nyasi na maua ni mimea inayovutia katika mazingira na kuyapendezesha. Pia, huleta hewa na harufu nzuri. Miti, nyasi na maua vikikosekana, mazingira huweza kuwa jangwa. Mandhari yenye harufu nzuri ya maua, huwavutia wadudu kama vipepeo na nyuki.

Soma mazungumzo ya Dotto na Baraka kuhusu hatua za kupanda miti, nyasi na maua.

**Dotto** Baraka nimepita shuleni kwenu nimekuta viunga vya nyasi, miti na maua. Vinapendeza sana.

**Baraka** Ni kweli, shuleni kwetu kuna bustani za maua, miti na nyasi. Inatuletea hewa safi na harufu nzuri.

**Dotto** Ooh! Mlianzaje kuwa na mazingira hayo?

**Baraka** Kwanza kabisa tulianza na wazo. Aina gani ya nyasi, maua na miti tunayotaka kupanda katika mazingira yetu.

**Dotto** Eehee! Nielekeze zaidi.

**Baraka** Hakikisha unachagua sehemu yenye rutuba kupanda nyasi, miti na maua.

**Dotto** Wazo zuri sana, nimelipenda.

**Baraka** Hatujafika mwisho, pia unatakiwa kusafisha eneo. Eneo liwe tayari kwa ajili ya upandaji wa miti, nyasi na maua.

**Dotto** Nazidi kufurahia elimu hii. Je, hatua gani zinafuata?

**Baraka** Unatakiwa kuboresha udongo kwa kuchanganya na mbolea kabla ya kupanda miche.

**Dotto** Jamani Baraka! Baada ya hapo mnafanyaje?

**Baraka** Tunalima eneo kwa kutifua na kuchagua miche tunayoihitaji, kisha tunapanda miche hiyo.

**Dotto** Kumbe! Ndio maana mazingira ya shule yenu yanavutia.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 12 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Baraka** Hata hivyo, tunatunza viunga vyetu kwa kumwagilia na kupalilia kila inapohitajika. Pia tunaweka dawa kwenye viunga vyote vya maua ili wadudu waharibifu wasiharibu.

**Dotto** Nashukuru kwa elimu yako. Nakuahidi nitakwenda kumueleza mwalimu wangu ili tutembelee shuleni kwenu na kujifunza zaidi.

**Kazi ya kufanya**

Chagua kazi mojawapo ya kutunza mazingira na uifanye shuleni.

(a) Kutengeneza bustani ya maua.
(b) Kumwagilia miti na maua ya shule.
(c) Kufanya usafi wa kina, kama kufagia, kudeki na kupalilia bustani za maua.
(d) Kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira.
(e) Kuondoa takataka shuleni.

## Faida ya mazingira safi

Shule yetu ina mazingira safi. Shule yenye mazingira safi hupendeza na kuvutia. Mazingira machafu huwa maficho ya wadudu na wanyama hatarishi. Wadudu na wanyama hao ni kama vile nzi, mbu, panya na nyoka. Viumbe hawa hupenda kujificha katika maeneo machafu. Ni muhimu kuishi kwenye mazingira safi. Mazingira safi huepusha maambukizi ya magonjwa ya kuhara, malaria na tauni. Pia, huepusha uharibifu wa vyakula mashambani na nyumbani. Tufanye usafi kwenye mazingira yanayotuzunguka ili kuepusha madhara yatokanayo na uchafu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 13 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vitendo vitatu vinavyochafua mazingira ya shule yako.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
2. Taja faida mbili za kufanya usafi wa mazingira ya shule.
   (a) ______ (b) ______ .
3. Taja madhara mawili ya kutofanya usafi wa mazingira ya shule.
4. Orodhesha viumbe watatu hatari wanaojificha katika maeneo machafu shuleni kwako.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______.
5. Taja vitendo viwili vinavyoweza kuboresha utunzaji wa mazingira ya shule yako. (a) ______ (b) ______.
6. Orodhesha vifaa viwili vinavyoweza kutumika katika shughuli za kutunza mazingira ya shule.
   (a) ______ (b) ______.

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

7. Vitu vinavyounda mazingira vimegawanyika katika makundi makuu mawili__________
   (a) Vitu vilivyo na uhai na visivyo na uhai.
   (b) Vitu vilivyo angani na vilivyo ardhini.
   (c) Vitu vizima na vilivyo nusu.
8. Uharibifu wa mazingira unaweza kusababisha________
   (a) ushindi kwa jamii.
   (b) kuenea kwa magonjwa.
   (c) kupatikana kwa hewa safi.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

**Bustani** eneo lililopandwa miti ya maua, matunda au mboga

**Dekio** kitambaa, gunia au ufagio wa kusafishia sakafu kwa maji

**Jangwa** eneo kubwa na kame ambalo huwa na mchanga na lisiloota nyasi wala miti

**Maficho** sehemu za kujificha

**Mazingira** vitu vyote vinavyomzunguka kiumbe katika maisha yake

**Tandabui** utando wa buibui

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 15 30/07/2021 11:39

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

# Hali ya hewa ya mazingira yetu

Katika sura hii utajifunza kuhusu hali ya hewa ya mazingira yako. Hali ya hewa inahusisha jotoridi, mvua, mawingu na upepo wa sehemu husika. Katika sura hii utajifunza kipengele kimoja tu cha hali ya hewa. Kipengele hiki kitahusu jotoridi la sehemu unayoishi. Utajifunza pia kipimo cha halijoto, mbinu za kujikinga na baridi na joto.

## Kubaini jotoridi katika mazingira yetu

### Maana ya jotoridi

Hali ya hewa inaweza kuwa ya joto au ya baridi. Hali hii huitwa jotoridi. Joto likiongezeka tunasema jotoridi liko juu na kunapokuwa na baridi jotoridi huwa chini.




**Kielelezo namba 1** Kipimajoto

Kuna umuhimu wa kufahamu jotoridi la sehemu unayoishi. Hii itakusaidia kupanga shughuli zako. Vilevile, itakuwezesha kuchagua nguo za kuvaa katika siku au kipindi husika. Jotoridi hupimwa kwa kifaa kinachoitwa kipimajoto.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jedwali la mavazi yanayovaliwa wakati wa baridi na wakati wa joto**

| Wakati wa baridi | Wakati wa joto |
|---|---|
| 1. Sweta<br>2. Mgolole<br>3. Jaketi<br>4. Blanketi | 1. Nguo nyepesi<br>2. Nguo za pamba |

**Athari za joto na baridi kwa wanyama na mimea**

Soma majigambo yafuatayo kati ya joto na baridi, kisha jibu maswali.

**Joto** Mimi ni joto, chanzo changu ni jua. Jua likiwa kali mimi huwa mkali pia. Nikifika tu baridi hutimua mbio.

**Baridi** Mimi ni baridi, kiboko ya joto nikifika tu joto huhama.

**Joto** Wee! Mimi nakausha maji ya mito, mabwawa na visima. Hata mazao nayakausha na kusababisha njaa. Mimi ni mwamba kuliko wewe.Tena ni kiboko yako, hata viumbe hujificha nikichachamaa.

**Baridi** Thubutu! Hunishindi mimi. Nikichachamaa viumbe hujikunyata. Hakuna kinachoweza kuishi. Wote wanaganda na kufa.

**Joto** Sio kweli, hata ukizidi watu wanajifunika na kuvaa nguo nzito ili kukudhibiti. Lakini mimi hata watu wasipovaa nguo wanatoka jasho na kukosa raha. Namaliza maji mwilini mwao na wanaweza hata kufa. Hata vyakula vyao vinaoza kwa sababu yangu mimi.

**Baridi** Wewe! Mawingu tu kiboko yako, yakitanda huna nguvu. Miti nayo ni kiboko yako. Hata ukijitutumua

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 17 30/07/2021 11:39


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

watu wanakaa kwenye vivuli chini ya miti na kustarehe. Wakiwa ndani wanajipulizia upepo kwa feni. Wanaweka vitu vyao kwenye jokofu na maisha yanaenda vizuri. Wewe joto si lolote.

**Joto** Sawa bwana, tusigombane. Sisi sote tuna faida tukiwepo kwa kiasi na hasara kama tukizidi sana.



**Kielelezo namba 2** Mavazi ya kujikinga wakati wa baridi



**Kielelezo namba 3** Mfano wa mavazi ya wakati wa joto

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 18 30/07/2021 11:39


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Chanzo cha joto ni nini?
2. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi kinaitwaje?
3. Joto kali lina athari gani kwa mimea na wanyama?
4. Taja njia mbili za kujikinga na hali ya hewa ya baridi kali.
5. Taja mbinu za kujikinga na hali ya hewa ya joto kali.

**Tazama picha ifuatayo, kisha jibu maswali.**




**Kielelezo namba 4** Wanafunzi wakisoma jotoridi kutoka kwenye kipimajoto

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Ni kifaa gani kinachoonekana katika picha?
2. Kifaa kinachoonekana katika picha kinatumika kufanyia nini?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

Toka nje ya darasa na usimame hapo kwa muda mfupi. Kisha ingia darasani na ukae. Je, umehisi mabadiliko yoyote ya joto mwilini? Waeleze wenzako kile ulichogundua.

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Eleza jotoridi la sehemu unayoishi.
2. Taja faida mbili za kujua jotoridi katika mazingira yako.

   (a) ______________ (b) ______________ .
3. Chora kifaa kinachotumika kupima jotoridi.
4. Andika **Ndiyo** kwa sentensi iliyo sahihi au **Hapana** kwa sentensi isiyo sahihi.

   (a) Joto na baridi huitwa jotoridi. ______________

   (b) Jotoridi kuwa juu au chini husababishwa na mwanga. ______________

   (c) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa kipima hewa. ______________

   (d) Mito na mabwawa hukauka kutokana na joto. ______________

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 20 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Chachamaa** | shikilia msimamo wa jambo |
| **Jokofu** | chombo kinachohifadhi vitu katika hali ya ubaridi ili visiharibike |
| **Jotoridi** | kiwango cha joto au baridi kilichoko katika hewa |
| **Kipimajoto** | chombo kinachotumika kupima jotoridi |
| **Kujikunyata** | kujikunja |
| **Majigambo** | hali ya kutoa maneno ya kujisifia |
| **Mgolole** | shuka nzito inayopitishwa juu ya mabega |
| **Feni** | kifaa kinachozalisha msukumo wa hewa |
| **Thubutu** | haiwezekani hata kidogo |
| **Tutumua** | vimbisha, tunisha |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 21 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Utamaduni wetu

Katika sura ya pili umejifunza hali ya hewa ya sehemu unayoishi. Umejifunza pia namna ya kujikinga na hali ya baridi na joto kali. Katika sura hii utajifunza matendo ya kudumisha utamaduni wa Kitanzania yakiwemo kusalimiana. Matendo mengine ni kucheza michezo ya kiutamaduni, kuimba nyimbo na kucheza ngoma.

### Kusalimiana kwa matendo mbalimbali

Watoto wenye tabia njema husalimiana. Vilevile, husalimia watu wazima wanaokutana nao hata kama hawafahamiani nao. Kila jamii ya Tanzania ina utamaduni wake. Baadhi ya mambo muhimu katika kudumisha utamaduni ni pamoja na kusalimiana.

Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 1** Namna mbalimbali za kusalimiana



FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 22 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Watu walioko katika picha wanasalimiana kwa namna gani?
2. Taja namna mbili nyingine za kusalimiana ambazo hazikuoneshwa kwenye picha.
   (a) ______ (b) ______.
3. Je, katika jamii yako watu wa rika mbalimbali wanasalimianaje?

Katika uchunguzi wa picha umeona namna mbalimbali za kusalimiana. Baadhi ya jamii husalimiana kwa kushikana mikono, mfano jamii za pwani. Jamii nyingine husalimiana kwa kubusiana mikono kwa mfano, Wahehe. Vilevile, zipo jamii kama za Wasukuma ambazo husalimiana kwa kupiga goti. Wengine husalimiana kwa kugongana mabega kama vile Wakinga.

## Zoezi la 2

Andika **Ndiyo** kwa sentensi iliyo sahihi au **Hapana** kwa sentensi isiyo sahihi.

1. Wakinga husaliamiana kwa kugongana mabega.________
2. Wazaramo husaliamiana kwa kupiga magoti.________
3. Wahehe husalimiana kwa kushikana mikono.________
4. Wasukuma husalimiana kwa kubusiana mikono.________

## Kazi ya kufanya

Mweleze mwenzako namna mnavyosalimiana katika jamii unayoishi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Namna ya kusalimiana kutokana na umri

Soma mazungumzo kati ya Tabasamu na Kiwandi, kisha jibu maswali.

**Tabasamu** Sisi nyumbani kwetu huwa tunasalimiana. Namna ya kusalimiana hutofautiana kutegemea umri.

**Kiwandi** Mmh! Nifundishe jinsi mnavyosalimiana nyumbani kwenu.

**Tabasamu** Watu wa umri mmoja wanapokutana wanasalimiana habari gani? au hujambo?

**Kiwandi** Aah! Hata kwetu huwa tunasalimiana hivyo.

Unayemsalimia huitikiaje?

**Tabasamu** Anayesalimiwa naye huitikia nzuri au sijambo, na wewe hujambo?

**Kiwandi** Jamani! hata binamu yangu nilimsalimia aliitikia hivyo.

**Tabasamu** Ila aliyekuzidi umri utamsalimia kwa adabu. Utasema shikamoo baba, mama, kaka au bibi.

**Kiwandi** Hee! Nao watakujibu vipi?

**Tabasamu** "Marahaba" mwanangu, mdogo wangu au mjukuu wangu.

**Kiwandi** Asante Tabasamu kwa kunielewesha namna ya kusalimiana.

Kusalimiana ni muhimu kwa sababu kunawezesha watu kujuliana hali kila wanapokutana. Pia, ni kiashirio cha tabia njema na kumuonesha mtu kuwa unamjali. Vilevile, kunawezesha mtu kupewa msaada stahiki endapo atakuwa na matatizo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Taja faida nne za kusalimiana katika jamii.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______.
2. Chora picha ya watu wakisalimiana.

## Kucheza michezo ya kiutamaduni

Kila jamii ina michezo yake ya asili kama sehemu ya kudumisha utamaduni. Jamii mbalimbali hucheza michezo ya asili kulingana na mazingira na shughuli wanazofanya.

Jamii za Kitanzania pia hucheza michezo mbalimbali ya kiutamaduni. Mchezo wa bao huchezwa zaidi na jamii za pwani. Michezo mingine ni kulenga shabaha, kurusha mkuki na mbio.

Malengo ya michezo hii ni kukuza uwezo wa kufikiri na kuamua. Aidha, hujenga umahiri wa kupambana na kujilinda na maadui. Malengo mengine ni kujenga ukakamavu na kuongeza ujuzi wa kufanya kazi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Taja malengo mawili mengine ya michezo ya kiutamaduni.
   (a) _______ (b) _______.
2. Taja michezo mitatu ya kiutamaduni ambayo haikutajwa katika habari. (a) _______ (b) _______ (c) _______.



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 25 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Taja michezo ya asili inayochezwa katika jamii yako.
4. Taja michezo minne ya kiutamaduni unayopendelea kucheza.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______.

**Oanisha sentensi za safu A na safu B ili kuleta maana.**

| **Na.** | **Safu A** | **Na.** | **Safu B** |
|---|---|---|---|
| 5. | Bao huchezwa na ___ | (a) | hujenga ukakamavu |
| 6. | Kurusha mkuki, kulenga shabaha____ | (b) | hudumisha utamaduni |
| 7. | Michezo _______ | (c) | jamii ya pwani |
| 8. | Michezo ya asili _______ | (d) | michezo ya kiutamaduni |
| | | (e) | kulenga shabaha |

## Kazi ya kufanya

Uliza watu wazima katika jamii yako kuhusu michezo ya kiutamaduni inayochezwa.

FOR ONLINE USE ONLY




Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 26 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuimba na kucheza ngoma

Jamii nyingi hushiriki katika kuimba nyimbo na kucheza ngoma za asili. Nyimbo na ngoma hizo ni njia nyingine ya kudumisha utamaduni wetu. Tunapocheza ngoma za utamaduni tunapata burudani. Vilevile, tunapata mazoezi ya mwili na kuleta hamasa katika shughuli mbalimbali.

Chunguza picha, kisha jibu swali.



**Kielelezo namba 2** Wanakijiji wakicheza ngoma ya utamaduni

### Swali

Je, ni vifaa vipi vinavyotumika kucheza ngoma unavyoviona katika picha?



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 27 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuimba na kucheza ngoma katika kijiji cha Uledi

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.

Wakiru ni wakazi wa kijiji cha Uledi pembezoni mwa milima ya Micheku. Wakazi wa kijiji hiki ni wakulima. Baada ya mavuno Wakiru huimba na kucheza ngoma ya asili iitwayo Mukirungu. Katika ngoma hiyo huimba nyimbo mbalimbali zinazohamasisha ushiriki katika shughuli za kilimo. Ngoma hii hupendwa na kuchezwa na watu wote, wakubwa kwa wadogo. Ni ngoma inayochezwa kila siku muda wa jioni.

Wakati wa kucheza ngoma ya Mukirungu, wanaume huvaa maleba kiunoni. Maleba hayo hutengenezwa kwa nyuzi za katani. Vifua vyao hubaki wazi. Kichwani huvaa taji lililotengenezwa kwa manyoya ya mbuni. Miguuni mwao huvaa njuga.

Wanawake huvaa kama wanaume, isipokuwa wao huvaa maleba vifuani mwao. Ngoma hupigwa kwa ustadi ambao huhamasisha kila mtu kujumuika kucheza. Wakati wa kucheza, wanaume hurukaruka kwa madaha. Wanawake huchezesha vichwa na vifua vyao.

### Zoezi la 5

**Jibu maswali haya.**

1. Taja matendo mawili yanayofanywa na Wakiru katika kudumisha utamaduni wao.
   (a) _______ (b) _______ .
2. Wakiru wanafanya shughuli gani?
3. Taja vifaa vitatu vinavyotumika katika kucheza ngoma ya Mukirungu. (a) _______ (b) _______ (c) _______ .
4. Ni ngoma gani umewahi kucheza katika jamii yako?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ngoma zinazochezwa na baadhi ya makabila ya Tanzania

Ngoma hutambulisha na kudumisha utamaduni wa jamii husika. Pia, husaidia kujenga umoja na ushirikiano miongoni mwao. Wanajamii wote huburudika na ngoma hizo. Katika jamii za Watanzania ngoma huchezwa katika nyakati mbalimbali.

Nyakati hizo ni za mavuno na sherehe kama harusi, jando na unyago. Baadhi ya ngoma za makabila ya Tanzania ni Mbeta inayochezwa na Waluguru. Mtingo na Iringi ambazo huchezwa na Wachaga. Wasukuma hucheza ngoma ya Bugobogobo na Beni.

Jamii ya Wasambaa hucheza Mdumange na Wangoni hucheza Lizombe. Mganda huchezwa na Wanyasa na Wamanda. Ngoma ya Kasimbo na Enchuma huchezwa na Wahaya. Sindimba huchezwa na Wamakonde na Mdundiko huchezwa na Wazaramo.

### Zoezi la 6

**Jibu maswali haya.**

1. Taja ngoma tatu za asili zilizotajwa kwenye habari.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
2. Taja ngoma mbili nyingine za asili unazozijua.
   (a) ______ (b) ______ .
3. Ni vifaa gani vinatumiwa katika kucheza ngoma ya asili ya kabila lako?

### Kazi ya kufanya

Imba na kucheza ngoma inayochezwa katika jamii unayoishi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 29 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja matendo manne yanayodumisha utamaduni wenu.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______ .
2. Taja faida mbili za kucheza ngoma za kiutamaduni.
   (a) _______ (b) _______ .
3. Orodhesha vifaa vinne vinavyotumika wakati wa kucheza ngoma za asili.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______ .
4. Chora watu wawili wakiwa wanacheza ngoma, wamevalia mavazi ya kuchezea ngoma.
5. Taja ngoma mbili za makabila mbalimbali unazozifahamu.
   (a) _______ (b) _______ .

## Msamiati

**Kudumisha** kuendeleza jambo

**Madaha** matendo na mwendo wa kupendeza

**Maleba** mavazi ya asili ya shughuli maalumu za kiutamaduni

**Njuga** kengele ndogondogo zinazofungwa miguuni, mikononi au shingoni wakati watu wanapocheza ngoma

**Utamaduni** mtindo wa jumla wa maisha ya jamii fulani

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 30 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne


## Uhusiano mwema

Utakumbuka kwamba katika sura ya tatu umejifunza matendo yanayodumisha utamaduni katika jamii. Katika sura hii utajifunza juu ya kujenga uhusiano mzuri. Uhusiano mzuri unaanza kwa kuwatambua watu unaoishi nao. Hivyo utajifunza, uhusiano wako na watu unaoishi nao katika familia. Aidha, utajifunza namna ya kujenga uhusiano mzuri na marafiki.

### Dhana ya familia

#### Familia ni nini?

Familia ni kikundi kidogo cha watu walio na uhusiano. Uhusiano wao unaweza kuwa wa damu, ndoa au wa kuishi pamoja.



**Kielelezo namba 1** Familia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Aina za familia

Hapa kwetu Tanzania kuna aina kuu mbili za familia. Aina hizo ni, familia ya awali na familia pana. Familia nyingine ni za mume na mke, familia ya mzazi mmoja, familia ya watoto yatima, familia ya makubaliano.

## Aina kuu za familia

### 1. Familia ya awali

Familia ya awali ni familia yenye baba, mama na watoto wao.



**Kielelezo namba 2** Familia ya awali




Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 32 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## 2. Familia pana

Familia hii ni kubwa zaidi. Ina watu wengi kuliko familia zilizotangulia. Familia pana inaweza kuwa baba, mama, watoto, babu, bibi, shangazi na mjomba.



**Kielelezo namba 3** Familia pana

## Aina nyingine za familia

### 1. Familia ya mzazi mmoja

Familia hii inaweza kuwa ya mama na watoto. Pia, inaweza kuwa ya baba na watoto. Familia ya namna hii huitwa familia ya mzazi mmoja.



**Kielelezo namba 4** Familia ya mzazi mmoja



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 33 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## 2. Familia ya mume na mke

Ni familia ya mume na mke waliooana ambao hawajapata mtoto. Familia hiyo huwa na idadi ya watu wawili.



**Kielelezo namba 5** Familia ya mume na mke

## 3. Familia ya watoto yatima

Ni familia ya watoto wanaoishi peke yao na kujitegemea bila ya wazazi. Hakuna mwanaukoo wala marafiki waliojitolea kuishi na watoto hawa.



**Kielelezo namba 6** Familia ya watoto yatima

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 34 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**6. Familia ya makubaliano**

Hii ni familia ya makubaliano kati ya watu wanaoishi pamoja. Mfano, mke na mume wanaolea watoto wa wenzao.

## Zoezi la 1

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Familia ni kikundi cha watu walio na ____________
   (a) chuki.
   (b) uhusiano. ( )
   (c) majigambo.

2. Kuna aina ____________ za familia.
   (a) tatu
   (b) nne ( )
   (c) sita

3. Familia yenye watu wengi huitwa ____________
   (a) familia ya awali.
   (b) familia pana. ( )
   (c) familia ya mume na mke.

4. ____________ ndiye kiongozi mkuu katika familia.
   (a) Baba
   (b) Kaka ( )
   (c) Mjomba


5. Familia inapaswa kuishi kwa upendo na ____________
   (a) kupigana.
   (b) kuheshimiana. ( )
   (c) kuombaomba.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kufahamu uhusiano na watu unaoishi nao katika familia

Soma mazungumzo ndani ya familia ya awali.












Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 36 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE









FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 7** Familia ya baba, mama na watoto wakiwa katika mazungumzo

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**


1. Baba wa mama yako unamwita nani?
2. Kaka wa mama yako unamwita nani?
3. Dada wa baba yako unamwita nani?
4. Mtoto wa mjomba wako unamwita nani?
5. Dada wa mama yako unamwita nani?
6. Kaka wa baba yako unamwita nani?



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 38 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chunguza mti wa familia, kisha jibu maswali.**




**Kielelezo namba 8** Mti wa familia

## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Familia yako ina idadi ya watu wangapi?
2. Chora mti wa familia yako. Weka majina ya ndugu zako, ndugu wa baba na mama yako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 39 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujenga uhusiano mzuri na marafiki

Kujenga uhusiano mzuri na wanafamilia ni muhimu. Aidha, ni vizuri kujenga uhusiano mzuri na marafiki. Rafiki ni mtu unayempenda na kumwamini asiyekuwa ndugu yako.

Angalia picha zifuatazo za vitendo vya uhusiano mwema na marafiki.



**Kielelezo namba 9** Kula chakula pamoja na rafiki




**Kielelezo namba 10** Hali ya mshikamano



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 11** Kusoma kwa pamoja



**Kielelezo namba 12** Kucheza kwa pamoja



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 41 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Katika picha ulizoona taja mambo mawili yanayofaa kuigwa.
   (a) ______ (b) ______ .
2. Andika matendo yanayodumisha uhusiano mzuri na marafiki uliyoyaona katika picha.
3. Taja faida mbili za kuwa na marafiki.
   (a) ______ (b) ______ .
4. Taja hasara nne za kuchagua marafiki wabaya.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ (d) ______ .
5. Orodhesha michezo inayochezwa katika picha ulizoona.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Chimbuko la familia linaanzia kwa______
   (a) babu na bibi.
   (b) baba na mama. (    )
   (c) shangazi na mjomba.
2. Viongozi wakuu wa familia ni______
   (a) baba na kaka.
   (b) babu na bibi. (    )
   (c) baba na mama.

## Kazi ya kufanya

Ni matendo gani yanayoweza kuvunja uhusiano kati yako na marafiki zako?

## Msamiati

**Uhusiano** hali ya kuwa na fungamano na mtu



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Viongozi wa nchi yetu

Katika sura ya nne umejifunza uhusiano wa watu katika familia. Vilevile, umejifunza namna ya kujenga uhusiano mwema na marafiki. Katika sura hii utawatambua viongozi wa nchi yetu. Aidha, utawatambua kwa majina na awamu zao za uongozi. Vilevile, utafahamu kazi walizofanya wakati wa uongozi wao.

### Viongozi wakuu wa Tanzania

Tanganyika ilipata uhuru wake tarehe 9 mwezi wa Disemba mwaka 1961. Tanzania ni muungano wa nchi mbili ambazo ni Tanganyika na Zanzibar. Nchi hizi ziliungana tarehe 26 mwezi wa Aprili mwaka 1964.

Tangu kuundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumekuwa na viongozi mbalimbali wa Serikali. Viongozi hao ni Marais na Mawaziri wakuu. Rais huchaguliwa na wananchi kwa kupigiwa kura. Waziri Mkuu huteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa wabunge waliochaguliwa na wananchi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 43 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Marais wa Tanzania tangu Muungano na mchango wao kwa Taifa**

| Mwaka | Awamu | Jina la Rais | Mchango kwa Taifa |
|---|---|---|---|
| 1964 – 1985 | Kwanza | Julius Kambarage Nyerere | • Aliongoza harakati za kudai uhuru.<br>• Alishiriki kuanzisha muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar.<br>• Kuasisi mfumo wa Ujamaa na kujitegemea.<br>• Kuasisi misingi ya elimu kwa wote.<br>• Kudumisha amani, umoja na mshikamano. |
| 1985 – 1995 | Pili | Ali Hassan Mwinyi | • Kuanzisha sera ya soko huria.<br>• Kuruhusu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi. |
| 1995 – 2005 | Tatu | Benjamin William Mkapa | • Kuongeza uwazi katika utendaji wa Serikali.<br>• Kuanzisha mfumo wa ubinafsishaji.<br>• Kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato ya Serikali. |
| 2005 - 2015 | Nne | Jakaya Mrisho Kikwete | • Kuboresha miundombinu mfano barabara na madaraja.<br>• Ujenzi wa shule za kata na vyuo vya elimu ya juu.<br>• Mapambano dhidi ya magonjwa mfano malaria na UKIMWI. |
| 2015 - 2021 | Tano | John Pombe Magufuli | • Elimu bure kwa wote, kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne.<br>• Kusimamia ulipaji kodi.<br>• Kupambana na ufisadi.<br>• Kupambana dhidi ya madawa ya kulevya.<br>• Kusimamia uwajibikaji katika sekta za umma. |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 44 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Majina ya Mawaziri wakuu wa Tanzania tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

| Mwaka | Awamu | Majina ya Mawaziri wakuu |
|---|---|---|
| 1972 - 1985 | Kwanza | 1. Rashidi Mfaume Kawawa<br>2. Edward Moringe Sokoine<br>3. Cleopa David Msuya<br>4. Salim Ahmed Salim |
| 1985 - 1995 | Pili | 1. Joseph Sinde Warioba<br>2. John Samwel Malecela<br>3. Cleopa David Msuya |
| 1995 - 2005 | Tatu | 1. Frederick Tluway Sumaye |
| 2005 - 2015 | Nne | 1. Edward Ngoyai Lowassa<br>2. Mizengo Kayanza Pinda |
| 2015 - | Tano | 1. Majaliwa Kassim Majaliwa |

Julius Kambarage Nyerere alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Serikali ya Tanganyika. Kuanzia tarehe 9 Disemba mwaka 1961 hadi tarehe 22 Januari mwaka 1962.

Kuanzia mwaka 1962 hadi mwaka 1972 hakukuwa na cheo cha Waziri Mkuu. Cheo hicho kilirudi tena mwaka 1972.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Marais wa Tanzania tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

Chunguza picha zifuatazo, kisha fanya zoezi.

1



2



3



4



5



**Kielelezo namba 1** Picha za Marais wa Tanzania tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 46 30/07/2021 11:40

Mawaziri wakuu wa Tanzania tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1


2


3


4


5


6


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7



8



9



10



**Kielelezo namba 2** Picha za Mawaziri wakuu wa Tanzania tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 48 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Andika katika daftari lako jina la Rais kulingana na namba ya picha.
2. Andika kwenye daftari lako jina la Waziri Mkuu kulingana na namba ya picha.
3. Chunguza,
   (a) Sarafu ya shilingi mia moja, ina picha ya Rais gani?
   (b) Noti ya shilingi elfu moja ina picha ya Rais gani?

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Ni Mawaziri wakuu wangapi walioongoza Tanzania?
2. Ni awamu zipi zilikuwa na Mawaziri wakuu zaidi ya mmoja?
3. Rais wa sasa anaitwa nani?
4. Waziri Mkuu wa sasa anaitwa nani?

## Kazi ya kufanya

Baada ya kusoma jedwali la viongozi wakuu wa Tanzania.
(a) Jadili katika vikundi habari za baba wa taifa la Tanzania.
(b) Simulia wenzako darasani habari za uongozi wa Rais wa kwanza wa Tanzania.

## Mchango wa viongozi wakuu wa Serikali ya Tanzania

Tanzania imeongozwa na viongozi wakuu mbalimbali katika awamu tofauti ambazo umeshazisoma. Viongozi wakuu hao wamekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika awamu za uongozi wao waliweza kulinda amani ya nchi. Vilevile, umoja na mshikamano katika jamii zetu za Tanzania umeimarishwa na viongozi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 49 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tunajivunia pia ulinzi na usalama unaosimamiwa na viongozi wetu. Aidha, maendeleo katika sekta za Afya na Elimu yamesimamiwa na viongozi wetu. Viongozi hao wametuongoza vyema, hivyo tuwaheshimu na kuwapenda.

## Kazi ya kufanya

Baada ya kusoma habari hii fanya yafuatayo. Tunga wimbo wa kuwasifia viongozi wakuu na kuimba darasani.

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja mambo ambayo ungependa viongozi wakuu wa Serikali walifanyie Taifa la Tanzania.
2. Taja michango ya viongozi wakuu katika taifa letu.
   (a) ______ (b) ______ .
3. Taja jina la Rais aliyeongoza Tanzania kwa muda mrefu kuliko wengine.

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Waziri Mkuu wa Serikali ya Awamu ya Tatu alikuwa______
   (a) Frederick Tluway Sumaye.
   (b) Jakaya Mrisho Kikwete. (    )
   (c) Mizengo Kayanza Pinda.
2. Baba wa taifa la Tanzania anaitwa ____________
   (a) Julius Kambarage Nyerere.
   (b) John Magufuli. (    )
   (c) Edward Sokoine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Ni vyema kuwaheshimu viongozi wetu wakuu kwa sababu__________
   (a) wametuletea amani na umoja.
   (b) wametuhesabu idadi yetu. ( )
   (c) wametukumbusha kazi za kufanya.

4. Tanganyika ilipata uhuru wake mwaka__________
   (a) 1964.
   (b) 2017. ( )
   (c) 1961.

## Msamiati

**Amani** hali ya usalama isiyokuwa na fujo au vita

**Awamu** kipindi maalumu katika utendaji wa uongozi fulani

**Mshikamano** hali ya watu kuwa na msimamo wa pamoja katika kutimiza lengo fulani

**Muungano** hali ya kuwa pamoja

**Rais** kiongozi mkuu wa nchi

**Sekta** mchepuo mmojawapo katika shughuli za kijamii kama vile elimu

**Taifa** watu wanaoishi katika nchi moja wakiunganishwa na utamaduni wao

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 51 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

# Kusoma ramani

Katika sura ya tano umejifunza majina ya Marais na Mawaziri wakuu wa Tanzania. Vilevile, umejifunza awamu zao walizoongoza Tanzania na mchango wao kwa Taifa letu. Katika sura hii utajifunza kuchora picha na ramani za vitu vilivyomo darasani.

## Kubaini vitu vilivyomo darasani

Soma mazungumzo kati ya Jenka na Nura, kisha jibu maswali.

**Nura** Habari Jenka.

**Jenka** Nzuri Nura.

**Nura** Darasani kwetu siku hizi kunapendeza.

**Jenka** Mmh! Kuna nini?

**Nura** Tumeletewa meza na viti vipya.

**Jenka** Darasani kwetu kuna kiti na meza ya mwalimu tu. Sisi tunakalia madawati.

**Nura** Pia, tuna ubao wa kuandikia.

**Jenka** Hata sisi tuna ubao.

**Nura** Sisi tumeletewa kabati la kutunzia vitabu, chaki na vifaa vingine tunavyotumia darasani. Ninyi mnalo?

**Jenka** Sisi hatuna kabati, vitabu vyetu vinatunzwa ofisini kwa mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Nura** Kuta za darasa letu zimepambwa kwa picha nyingi na ramani. Baadhi ya picha tumezichora wenyewe na nyingine zimeletwa na mwalimu.

**Jenka** Sisi tuna picha chache tu lakini hatuna ramani.

**Nura** Aha! Sisi tuna tenga la plastiki kwa ajili ya kuweka takataka. Hivyo darasa letu huwa safi wakati wote.

**Jenka** Sisi hatuna tenga ila tunahifadhi uchafu kwenye boksi. Boksi likijaa tunakwenda kutupa kwenye shimo la takataka. Zaidi ya hapo tuna rula kubwa ya kupigia mistari ubaoni. Ninyi mnayo?

**Nura** Ndiyo, hata sisi tunayo. Vitu hivi vinatusaidia kujifunza vizuri.

## Zoezi la 1

1. Vitu gani vilivyoko darasani kwako ambavyo havikutajwa kwenye mazungumzo ya Jenka na Nura?
2. Je, vitu gani muhimu vinavyotakiwa kuwepo darasani lakini kwenye darasa lako havipo?

FOR ONLINE USE ONLY




Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 53 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuchora picha za vitu vilivyomo darasani

Chunguza picha, kisha jibu maswali.

(a)




(b)




(c)



(d)




(e)



(f)



**Kielelezo namba 1** Picha za vitu vilivyomo darasani

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 2

1. Andika majina ya vitu vinavyoonekana katika picha (a - f ).
2. Chora picha ya vitu sita vilivyomo darasani kwako.


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuchora ramani za vitu vilivyomo darasani

Tumeona kuwa picha ni mchoro wa kitu kama kinavyoonekana kikiwa mbele yako. Hivyo picha huwakilisha sura ya kitu halisi. Hata hivyo tunaweza kutumia aina nyingine ya mchoro kuwakilisha kitu halisi. Mchoro huo hujulikana kama ramani.

### Michoro ya picha na ramani

Chunguza safu ya michoro, kisha fuata maelekezo.




**Kielelezo namba 2** Picha na ramani za vitu vilivyomo darasani

### Zoezi la 3

Eleza tofauti ya picha na ramani za vitu vilivyoko katika kielelezo namba 2.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tofauti kati ya vitu halisi, picha na ramani

Jedwali lifuatalo linaonesha tofauti kati ya vitu halisi, picha na ramani.

| Tofauti | Vitu halisi | Picha | Ramani |
|---|---|---|---|
| Uhalisia | Vinaonesha umbo halisi la kitu kama kinavyo onekana kutoka pande zote. Yaani vina urefu, upana na kimo. | Inaonesha umbo la kitu kama kinavyoonekana kikiwa mbele yako. Picha huonesha umbo bapa lenye urefu na upana. | Inaonesha umbo la kitu kama kinavyoonekana kutoka juu. Ramani huonesha umbo bapa lenye urefu na upana. |
| Ukubwa | Vina ukubwa halisi. | Ukubwa haulingani na ukubwa halisi wa kitu. Picha inaweza kuwa kubwa au ndogo kuliko kitu halisi. | Ukubwa haulingani na ukubwa halisi wa kitu au eneo. Mara nyingi ramani inakuwa ndogo. |
| Upatikanaji | Hupatikana katika mazingira. | Huchorwa kwa mkono au kupigwa kwa kamera. | Inachorwa kwa mkono kwenye karatasi, ardhi au sehemu yoyote bapa. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Jinsi ya kuchora ramani

Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali.

**Mwalimu** Niliwaambia mchore ramani ya meza lakini wewe umechora picha ya meza.

**Mwanafunzi** Mwalimu, ulitufundisha kuwa ramani ni mchoro wa kitu. Na mimi nimechora mchoro wa meza.

**Mwalimu** Sawa, ramani ni mchoro lakini unakumbuka tulijifunza kuwa picha ni nini?

**Mwanafunzi** Tulijifunza kuwa picha ni mchoro wa kitu kinavyoonekana.

**Mwalimu** Sawa kabisa, lakini kitu hicho kinavyoonekana ukikiangalia kutoka wapi?

**Mwanafunzi** Aah! Kweli nimekumbuka, ukikiangalia kutoka mbele yako.

**Mwalimu** Ehee! Sasa hebu angalia hii meza kutoka juu. Unaona nini?

**Mwanafunzi** Ninaona sehemu ya juu tu ya meza. Sioni miguu yake.

**Mwalimu** Sawa kabisa, sasa umegundua kosa lako?

**Mwanafunzi** Ndiyo, nilitakiwa nichore sehemu ya juu ya meza ambayo ingeonekana kama mstatili. Sikutakiwa kuchora miguu ya meza.

**Mwalimu** Vizuri sana. Sasa unaweza kutofautisha ramani na picha?

**Mwanafunzi** Ndiyo mwalimu. Picha ni mchoro wa kitu kama unavyokiona mbele yako. Vilevile, ramani ni mchoro wa kitu kama unavyokiona ukikiangalia kutoka juu. Hivyo ramani huonesha sehemu ya juu tu. Haioneshi kimo cha kitu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 57 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Ramani ni nini?
2. Kuna tofauti gani kati ya picha na ramani?

## Zoezi la 5

**Jibu maswali haya.**

1. Chora ramani ya darasa kuonesha vitu vilivyomo.
2. Chora ramani ya ubao, kikombe na chupa.
3. Chora picha na ramani ya nyumba yenu.
4. Orodhesha vitu vilivyomo katika nyumba yenu lakini havionekani katika picha ya nyumba.
5. Taja vitu vinavyoonekana katika picha ya nyumba yenu lakini havionekani katika ramani.
6. Chora jedwali kuonesha picha na ramani za vitu hivi.

   mti, bilauri, meza, ndoo, sahani, kiti na kitabu.

## Kazi ya kufanya

Ramani za vitu zina matumizi gani katika maisha ya kila siku?

## Msamiati

**Kamera** kifaa cha kupigia picha

**Picha** mchoro wa kitu kama kinavyoonekana kwa mbele yako

**Ramani** mchoro wa kitu kama kinavyoonekana kutoka juu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Mfumo wa jua


Katika sura ya sita umejifunza kuchora picha. Pia, kuchora ramani za vitu vilivyomo darasani. Katika sura hii utajifunza vitu vinavyounda mfumo wa jua.

### Vitu vinavyounda mfumo wa jua

Mfumo wa jua ni utaratibu wa sayari kulizunguka jua. Sayari ni gimba linaloumbwa na miamba ambalo huzunguka jua kupitia njia maalumu.

### Sayari zinazounda mfumo wa jua

Chunguza picha, kisha jibu maswali.




**Kielelezo namba 1** Mfumo wa jua

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 59 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Taja sayari tatu unazoziona katika picha.

   (a) __________ (b) __________ (c) __________ .

2. Dunia ni sayari ya ngapi katika mfumo wa jua?
3. Kausi ni sayari ya ngapi kwenye mfumo wa jua?

## Kufafanua vitu vinavyounda mfumo wa jua

Mfumo wa jua umezungukwa na Sayari nane. Sayari hizo ni Zebaki, Zuhura, Dunia, Mirihi, Sumbula, Sarateni, Zohali na Kausi. Vilevile, kwenye mfumo wa jua kuna vitu vingine kama Asteroidi, Kometi na Meteroidi. Jua nalo ni sehemu ya mfumo huo.

Jua ni muhimu katika maisha ya kila siku. Jua hutupatia mwanga mchana. Pia, hukausha mazao na nguo. Vilevile, jua husababisha mazao kukua. Hakika mfumo wa jua hutupatia faida nyingi.

### Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Taja faida tatu za jua.

   (a) __________ (b) __________ (c) __________ .

2. Vitu gani vingine vinapatikana kwenye mfumo wa jua?
3. Taja sayari tatu zinazolizunguka jua.

   (a) __________ (b) __________ (c) __________ .

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 60 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chunguza picha, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 2** Moja ya faida za jua

## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Taja mambo matatu yanayoweza kufanywa wakati wa jua.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

2. Ni faida gani ya jua unayoiona kwenye picha? ______
   (a) jua linapeperusha nguo zilizoanikwa.
   (b) jua linalowanisha nguo zilizoanikwa. ( )
   (c) jua linakausha nguo zilizoanikwa.

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na mwenzio kujua aina za gesi zinazopatikana kwenye sayari Dunia.

## Msamiati

**Gimba** umbile la kitu kama kilivyo



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kutunza rasilimali zetu

Katika sura ya saba umejifunza vitu vinavyounda mfumo wa jua. Katika sura hii utajifunza rasilimali zinazomilikiwa na familia na zinazomilikiwa na shule. Pia, utabaini faida za rasilimali na namna ya kuzitunza.

### Kubaini na kutunza rasilimali za familia yetu

Rasilimali ni vitu tulivyonavyo katika familia ambavyo tunavitumia ili tuweze kupata maendeleo. Vitu hivyo ni mifugo, ardhi, mazao na vyombo vya nyumbani.

### Utunzaji wa rasilimali

Soma mazungumzo kati ya Pamoa na Pilika, kisha jibu maswali.

**Pamoa** Habari yako Pilika.

**Pilika** Nzuri Pamoa.

**Pamoa** Jana nilikuona na ndoo, ulikuwa unakwenda wapi?

**Pilika** Nilikuwa nakwenda kuchota maji.

**Pamoa** Aha! Kwetu kuna bomba la maji. Maji ya bomba tunayatumia kupikia chakula, kufanya usafi na kumwagilia bustani.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 62 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Pilika** Hata kwetu kulikuwa na bomba, lakini ankara ikawa kubwa tukashindwa kulipia. Hivyo maji yakakatwa.

**Pamoa** Oh! Poleni, sisi tunahakikisha maji hayamwagiki ovyo kwa kufunga mabomba vizuri. Pia, tunakinga maji kwa uangalifu katika vyombo tunapotaka kutumia.

**Pilika** Aah! Nimejifunza kitu. Nami nitamwambia baba alipe ankara. Nitawashauri watu wa nyumbani kwetu tutumie maji vizuri. Lakini hata kwetu kuna shamba la miti. Linatupatia matunda, mbao na kuni.

**Pamoa** Ooh! Hata sisi tuna shamba lenye mazao ya chakula na biashara. Tunapata chakula na fedha kutokana na shamba hilo.

**Pilika** Sisi kwetu tuna mifugo. Tunapata maziwa, nyama na mbolea kutokana na mifugo hiyo.

**Pamoa** Hata sisi tunafuga kuku.Tunapata nyama, mayai na mbolea.

**Pilika** Kwetu kuna baiskeli, inatusaidia kusafirishia maziwa kwa ajili ya kwenda kuuza.

**Pamoa** Hongera! Kwetu kuna gari, tunalitumia kusafirishia mayai na kuku. Wakati mwingine tunalitumia kusafirisha mazao ya shambani kwenda kuuza.

**Pilika** Kumbe mna rasilimali zote hizo! Kwetu baadhi ya wanafamilia hutumia vibaya rasilimali zetu. Mfano, kuuza mifugo yetu bila idhini ya familia. Hivyo zimeanza kupungua.

**Pamoa** Hata kwetu wakati mwingine baadhi ya wanafamilia hutumia vibaya rasilimali zetu. Wengine hudiriki hata kuiba baadhi ya rasilimali za familia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Pilika** Hata hivyo, tunajitahidi kuzitunza rasilimali hizi kwa kuzikarabati. Aidha, tunawaelimisha wanafamilia jinsi ya kuzitumia na kuweka ulinzi ili zisiibwe.

**Pamoa** Kwetu pia kila mara tunatunza rasilimali hizi kwa kuzitumia kwa uangalifu. Pia, tunafuga mbwa wakali wa kutusaidia kuzilinda.

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Taja rasilimali nne zilizotajwa katika mazungumzo kati ya Pamoa na Pilika.
   (a) ______
   (b) ______
   (c) ______
   (d) ______ .

2. Taja vitendo vitatu vilivyotajwa katika mazungumzo vinavyoonesha matumizi mabaya ya rasilimali.
   (a) ______
   (b) ______
   (c) ______ .

FOR ONLINE USE ONLY




Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 64 30/07/2021 11:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kubaini rasilimali za familia

Chunguza picha, kisha jibu maswali.





**Kielelezo namba 1** Rasilimali za familia ya mzee Paulo



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 65 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Taja rasilimali nne zilizopo katika familia ya mzee Paulo.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______ .
2. Taja rasilimali zilizopo katika familia yenu.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ .
3. Taja faida mbili zinazopatikana kutokana na rasilimali za familia yenu.
   (a) _______ (b) _______ .
4. Taja njia mbili mnazotumia kutunza rasilimali za nyumbani kwenu.
   (a) _______ (b) _______ .

## Kazi ya kufanya

Taja njia nne ulizotumia kuhakikisha rasilimali zinatumika vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY




Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 66 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kubaini na kutunza rasilimali za shule yetu

Kama ilivyokuwa katika familia zetu, tunazo rasilimali mbalimbali shuleni kwetu.

Chunguza picha, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 2** Rasilimali za Shule ya Msingi Kiwandani

### Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Taja rasilimali sita zinazoonekana katika picha.
   (a) ___ (b) _____ (c) _____ (d) _____ (e) _____ (f) _____ .
2. Taja rasilimali zinazopatikana katika shule yako.

### Kazi ya kufanya kwa vikundi

Jadiliana na wenzako njia mbalimbali za kutunza rasilimali za shule yenu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Rasilimali za Shule ya Msingi Jitegemee

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Mimi ninaitwa Baraka. Ninasoma darasa la tatu katika Shule ya Msingi Jitegemee. Shuleni kwetu tuna rasilimali mbalimbali. Tuna majengo mazuri, madawati, ardhi nzuri, vitabu, kabati na meza. Vilevile, tuna gari, ng'ombe wa maziwa na duka.

Aidha, tuna shamba la miti na bomba la maji. Tunatumia maji kumwagilia bustani ya shule, kufanyia usafi na kunywesha mifugo. Tunatumia gari la shule kubeba majani ya ng'ombe, maziwa na mbao. Miradi hii inatusaidia kuongeza kipato cha shule. Vilevile, tunapata ujuzi wa kuendesha miradi ya uzalishaji. Rasilimali za shule yetu tunazitunza na kuzifanyia ukarabati wa mara kwa mara. Ng'ombe tunawatunza kwa kuwalisha vizuri na kuwatibu wanapopata magonjwa.

Mwalimu Juma husimamia duka la shule. Anahakikisha bidhaa haziibwi dukani wala duka halipati hasara. Walimu wetu wanahakikisha maji hayamwagiki ovyo kwa kukarabati mabomba. Madawati yakiharibika yanatengenezwa. Kila mwanafunzi ni mlinzi wa mwenzake katika kulinda rasilimali za shule. Hii inasaidia kulinda rasilimali za shule ili zisiibwe wala kuharibiwa. Rasilimali za shule yetu zina manufaa makubwa kwetu hivyo tuzitunze vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Shule ya Jitegemee ina rasilimali gani?
2. Taja vitendo vitatu vya utunzaji wa rasilimali vilivyoelezwa katika habari uliyosoma.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
3. Shule ya Jitegemee ina shughuli gani za uzalishaji mali? Zitaje. (a) ______ (b) ______ (c) ______ .



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 68 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

**Jibu maswali haya.**

1. Taja rasilimali mbili zilizopo shuleni kwenu ambazo hazipo nyumbani kwenu.
   (a) _______ (b) _______ .
2. Taja vitendo vitatu vinavyochangia katika uharibifu wa rasilimali za shule yenu.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ .
3. Pendekeza njia nne za kulinda rasilimali za shule yenu.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______ .

**Jaza nafasi zilizo wazi katika maswali haya.**

4. Matendo yanayochangia uharibifu wa rasilimali za familia ni ___________ na ___________ .
5. Mifugo, ardhi na mazao ni mifano ya ___________.

## Msamiati

**Ankara** orodha ya huduma iliyotolewa na fedha inayodaiwa

**Kukarabati** tengeneza upya kitu kilichoharibika

**Mifugo** wanyama wanaofugwa nyumbani

**Rasilimali** jumla ya mali aliyo nayo mtu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Uzalishaji mali

Katika sura ya nane umejifunza kubaini na kutunza rasilimali za familia na shule. Katika sura hii utajifunza shughuli za uzalishaji mali katika familia. Pia, utajifunza wajibu wa kila mwanafamilia katika shughuli za uzalishaji mali.

### Kutambua shughuli za uzalishaji mali katika familia

Tunahitaji chakula, mavazi na nyumba ili tuweze kuishi. Tutaweza kupata mahitaji hayo ya msingi kama tutafanya kazi kwa bidii. Kufanya kazi kwa ajili ya kupata mahitaji hayo huitwa uzalishaji mali. Shughuli kama uvuvi, ufugaji na kilimo zinaitwa shughuli za uzalishaji mali.

Katika kufanya shughuli hizo watu hupata chakula na fedha. Vivyo hivyo, tunalima ili kupata chakula. Pia, tunauza mazao ili kupata fedha za mahitaji. Mahitaji hayo ni kama vile kununulia nguo na kujenga nyumba.

Kila familia huwa na mahitaji ya kila siku. Katika kupata mahitaji hayo familia nyingi hushirikiana katika shughuli za uzalishaji mali.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 70 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kubaini shughuli za uzalishaji mali

Chunguza picha, kisha jibu maswali.





**Kielelezo namba 1** Watu wakifanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali

### Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Taja shughuli tatu zinazofanyika katika picha ulizoona.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
2. Shughuli zinazofanyika katika picha ulizoona zina faida gani?



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 71 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shughuli za uzalishaji mali katika familia

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.

Familia ya bwana na bibi Chapakazi wanaishi katika kitongoji cha Matumaini. Kitongoji hiki kipo nje kidogo ya mji wa Tupendane. Bwana Chapakazi ni mwalimu katika Shule ya Msingi Maendeleo. Bibi Chapakazi ni muuguzi katika zahanati ya Amani. Watoto wao Tumaini, Faraja na Upendo wanasoma Shule ya Msingi Maendeleo.

Baada ya kutoka kazini na shuleni, familia hii hujishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Shughuli hizo ni bustani ya mboga, ufugaji wa kuku wa mayai, kilimo na duka. Katika duka lao wanauza vyakula, sabuni, mafuta na vifaa vya shule.




**Kielelezo namba 2** Tumaini na Faraja wakilisha kuku



FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 72 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 3** Bwana Chapakazi akifanya shughuli ya uzalishaji mali

Bwana na bibi Chapakazi wakirudi nyumbani hufanya kazi katika bustani ya mboga. Wanauza mboga hizo ili kuongeza kipato cha familia.

Faraja na Tumaini wakirudi kutoka shuleni hulisha kuku na kukusanya mayai. Mayai yanatumika kwa chakula katika familia na mengine huuzwa ili kupata fedha. Wakati Faraja na Tumaini wakilisha kuku, Upendo huuza duka. Familia ya bwana na bibi Chapakazi hulima mazao ya chakula pia. Wakati wa kupanda mahindi baba na mama huchimba mashimo. Wototo wote hushiriki kuweka mbegu na kuzifukia.

Familia hii inasifika kwa mafanikio yanayotokana na ushirikiano. Vilevile, husifika katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 73 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Taja shughuli tatu za uzalishaji mali zilizotajwa katika habari hii.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ .
2. Taja wajibu wa kila mwanafamilia kama ifuatavyo.
   (a) Bwana Chapakazi na bibi Chapakazi.
   (b) Faraja na Tumaini.
   (c) Upendo.
3. Habari uliyosoma inakufundisha nini?

## Kazi za kufanya

1. Andika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinazoweza kufanyika katika familia yenu.
2. Wasimulie wenzako namna unavyoshiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwenye familia yenu.

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Orodhesha shughuli mbili za uzalishaji mali zinazofanyika katika familia yenu.
2. Eleza madhara matatu ya kutoshirikiana katika kazi za uzalishaji mali. (a) _______ (b) _______ (c) _______ .
3. Taja shughuli nne za uzalishaji mali zinazofanyika katika sehemu unayoishi.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______ .

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 74 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi za kufanya

Nini kitatokea iwapo hatutashiriki katika shughuli za uzalishaji mali?

## Msamiati

**Kipato** mavuno au fedha anazopata mtu zikiwa faida ya mauzo ya kitu

**Mali** kitu chenye thamani anachokimiliki mtu

**Muuguzi** mtu anayefanya kazi ya kuhudumia wagonjwa

**Uzalishaji mali** kufanya kazi au shughuli inayoleta kipato

**Zahanati** mahali pa kutolea matibabu kwa wagonjwa

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 75 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kutambua fursa katika maeneo mbalimbali

Katika sura ya tisa umejifunza shughuli za uzalishaji mali katika familia. Umejifunza pia wajibu wa kila mwanafamilia katika shughuli za uzalishaji mali. Katika sura hii utajifunza fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo yatajumuisha fursa za ardhi yenye rutuba na mvua nyingi.

### Kubaini fursa za shughuli za uzalishaji mali katika maeneo mbalimbali

Shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na jamii hutegemea fursa zilizopo katika mazingira. Watu wanaoishi sehemu zenye misitu hupasua mbao na kutengeneza samani. Wale wanaoishi sehemu zenye mito, maziwa na bahari huvua na kuuza samaki. Katika sehemu zenye mkusanyiko mkubwa wa watu kuna fursa ya kufanya biashara.

Watu wanaoishi sehemu zenye mvua wana fursa ya kufanya shughuli za kilimo. Shughuli hizi za uzalishaji mali huitwa pia shughuli za kiuchumi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutambua fursa zilizopo katika maeneo yenye rutuba

Chunguza picha, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 1** Mtu akishiriki shughuli za kilimo sehemu zenye rutuba

### Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Taja zao linaloonekana katika picha.
2. Shughuli inayoonekana katika picha ina faida gani?
   (a) ______
   (b) ______
   (c) ______ .

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kubaini fursa zilizopo kwenye ardhi

Soma shairi lifuatalo, kisha fanya zoezi.

Ardhi yenye rutuba,
hutoa kingi chakula,
Nafaka, mboga, matunda,
Miili yetu kujenga.

Biashara hufanyika,
Kwa mazao kuuzika,
Kupata kingi kipato,
Maisha kuendelea.

Kufuga hakuko nyuma,
Majani yakiwa mengi,
Maziwa nyama na ngozi,
Hupatikana kwa wingi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Taja fursa tatu zilizopo katika maeneo unayoishi.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______.
2. Taja fursa tatu zilizopo katika sehemu zenye rutuba.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______.
3. Taja mazao manne yanayopatikana katika maeneo yenye rutuba.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______.
4. Taja faida nne za ufugaji.
   (a) _______ (b) _______ (c) _______ (d) _______.



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 78 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutambua fursa zilizopo katika maeneo yenye mvua

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.

Siku moja Sikujua na mama yake walikuwa wanatoka shambani kulima. Walipochoka kutembea waliamua kupumzika chini ya mti. Giza lilianza kuingia. Sikujua akamuuliza mama yake, "Mama mbona giza limeingia mapema?''

Mama yake akamjibu kwa furaha kuwa, mawingu yametanda na karibu mvua itanyesha. Sikujua akamuuliza tena, "Mbona umefurahi, unapenda mvua? Mimi siipendi maana itanilowanisha wakati wa kwenda shule. Inaweza hata kuleta mafuriko na kuvunja daraja letu''. Mama akamwambia, "Mwanangu tunahitaji sana mvua, mvua inatusaidia kukuza mazao yetu. Bila mvua hatuwezi kupata chakula".

Sikujua akadakia, ''Ah! Si tutanunua chakula?'' Mama akasema, "Ndiyo tunaweza kununua lakini kama mvua haikunyesha chakula cha kununua kitatoka wapi?" Sikujua akasema, "Kweli mvua ni muhimu". Mama akaongeza, " Pia, mvua inaotesha majani kwa ajili ya mifugo yetu".

Sikujua naye akaongeza, "Na mimi nimekumbuka mama, mvua ikinyesha tunavuna maji. Pia, huwauzia watu wengine na kupata fedha". Mama akasema, "Unakumbuka mwaka jana kipindi cha mvua tulikamata senene wengi sana?" Sikujua akasema, "Ndiyo nakumbuka tulikula sana senene na wengine tukawauza. Kweli mvua inatupatia fursa nyingi sana".

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Taja faida nne za mvua zilizotajwa katika hadithi uliyosoma. (a) ______ (b) ______ (c) ______ (d) ______ .
2. Taja madhara ya mvua nyingi.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
3. Taja fursa tatu zinazopatikana sehemu zenye mvua.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja madhara matatu ya ardhi iliyokosa rutuba.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ .
2. Taja faida nne zitokanazo na shughuli za kiuchumi katika maeneo yenye mvua na ardhi yenye rutuba.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ (d) ______ .
3. Taja fursa nne za uzalishaji mali zinazopatikana sehemu unayoishi.
   (a) ______ (b) ______ (c) ______ (d) ______ .

FOR ONLINE USE ONLY

## Msamiati

**Fursa** nafasi ya kuweza kufanya jambo

**Samani** vyombo vya nyumbani kama vile meza, viti, kabati na vitanda vilivyotengenezwa kwa mbao

**Senene** panzi wa rangi ya kijani ambao hutumika kama kitoweo kwa baadhi ya makabila nchini



Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 80 30/07/2021 11:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Jaribio

**Sehemu A: Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Jotoridi hupimwa kwa kifaa maalumu kiitwacho________
   (a) rula. ( )
   (b) kipimajoto.
   (c) moto.

2. Jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu huitwa ____________
   (a) mazingira. ( )
   (b) kitanda.
   (c) mvua.

3. Chanzo cha asili cha joto ni ____________
   (a) mvua.
   (b) mawingu. ( )
   (c) jua.

4. Mtoto wa mjomba anaitwa ____________
   (a) shangazi.
   (b) binamu. ( )
   (c) mama mdogo.

5. Jambo mojawapo la kudumisha utamaduni wa Kitanzania ni kama vile______________
   (a) kuimba nyimbo.
   (b) kuvuta bangi. ( )
   (c) kuiba mifugo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu B:** Andika **Ndiyo** kwa sentensi iliyo sahihi, au **Hapana** kwa sentensi isiyo sahihi.

6. Mvua husaidia kukuza mazao.___________
7. Fagio na jembe ni vifaa vinavyotumika katika utunzaji wa mazingira. ___________
8. Sweta na jaketi ni mavazi yanayovaliwa wakati wa baridi. ___________
9. Mifugo na ardhi ni rasilimali. ___________
10. Nyota na mwezi huonekana wakati wa mchana. _______

**Sehemu C: Jaza nafasi zilizoachwa wazi.**


11. Vifaa vya kufanyia usafi darasani ni ___________, ___________ na ___________ .
12. Rais wa awamu ya kwanza aliitwa ___________ .
13. Rais wa awamu ya tano ni ___________ .
14. Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanzania aliitwa ________ .
15. Tanzania ni muungano wa Tanganyika na __________ .
16. Tanganyika imepata uhuru wake mwaka ___________ .
17. Rais wa awamu ya pili aliitwa ___________ .
18. Chora ramani ya darasa kuonesha meza ya mwalimu, ubao na madawati.
19. Taja rasilimali zinazopatikana shuleni.
    (a) _______________
    (b) _______________
    (c) _______________ .
20. Orodhesha majina ya Mawaziri wakuu wa Tanzania tangu Serikali ya awamu ya pili.





Maarifa ya jamii 3 1 March 2018 Final.indd 82 30/07/2021 11:41


## Vitabu kutoka
## Taasisi ya Elimu Tanzania


### Darasa la Tatu





ISBN 978-9987-09-317-5

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*